Tamthlia

Kithaka wa Mberia : Kifo Kisimani

Jibu swali 2 au 3.

1. **Fafanua** juhudi zilizofanywa na wanabutangi. Kupigania ukombozi wao na vizingiti walivyokumbana navyo katika kuutafuta ukombozi huo. (Alama 20)
2. " Niliambiwa nataka sana kumwona ili kumwomba msamaha na pia kumpa pole kwa mkasa uliomkumba."

   (i) **Fafanua** muktadha wa dondoo hili (alama 4)

   (ii) Anayetarajiwa ' kuonwa' katika dondoo hili amerundikiwa tuhuma si kidogo. **Fafanua**. (alama 4)

   (iii) **Eleza** ujinga unaodhihirishwa na msemaji wa maneno haya katika tamthlia. (alama 5)

   (iv) **Ni nini** hatima ya mazungumzo haya? (alama 7)

HADITHI FUPI

K. W. WAMITILA: Mayai Waziri wa maradhi

Jibu swali la 4 au la 5.

3. Ukimbizi ni swala sugu katika nchi nyingi. **Fafanua** asili na athari zake ukizingatia hadithi ya mkimbizi (alama 20)

Ngome ya Nafsi

4. Marahaba Mwanangu. Nikusaidie na nini?

   (i) **Fafanua** muktadha wa maneno haya (alama 4)

   (ii) Mzungumzaji alimpa msaada gani? (alama 4)

   (iii) Ni masaibu gani yaliyokuwa yamemkumba mzungumziwa? (alama 6)

   (iv) **Taja** haki zozote mbili ambazo msemewa amenyang'anywa (alama 2)

   (v) Mwanamume amechorwa vipi katika hii hadithi. (alama 4)

FASIHI SIMULIZI

6. (a) (i) **Eleza** maana ya misimu (alama 1)

   (ii) Kuchipuka kwa misimu kunategemea mambo mengi. **Taja** matano miongoni mwa haya. (alama 5)

   (iii) **Eleza** muhimu wa misimu katika jamii (alama 4)

   (b) (i) Nini maana ya ngomezi? (alama 2)

   (ii) Ngomezi ina umuhimu gani? (alama 5)

   (iii) **Taja** udhaifu wa ngomezi katika kuwasilisha ujumbe katika jamii (alama 3)

7. ***Soma mashairi haya kisha ujibu maswali yanayofuata***.

Shairi A

Umekata mti mtima
Umeangukia nyumba yako
Umeziba mto hasira
Nyumba yako sasa mafurikoni
Na utahama
Watoto kuwa kimbia.

Mbuzi kumkaribia chui
Alijigeuza panya
Akalia kuliwa na paka kichwani
Mchawi kutaka sana kutisha
Alijigeuza samba
Akalia na risasi kichwani

Jongoo kutaka sana kukimbia,
Aliomba miguu elfu
Akaachwa na nyoka

Hadija wapi sasa utakwenda
Bwanako kumpa sumu?
Hadija umemshika nyoka kwa mkia,
Hadija umepita nyama ya Punda.

Shairi B

Piteni jamani, Piteni haraka
Nendeni, nendeni huko mwendako
Mimi haraka, haraka sina,
Mzigo wangu, mzigo mzito mno
Na chini sitaki kuweka.

Vijana kwa nini hampiti?
Kwa nini mwanicheka kisogo?
Mzigo nilioubeba haupo kichwani
Lakini umenipinda mgongo na miguu
Na lazima nijiegemeze, kichwani
Chini nendeko.

Haya Piteni! Piteni! Haraka! Heei!
Mwafikiri mwaniacha nyuma!
Njia ya maisha ni moja tu
Huko mwendako ndiko nilikotoka
Na nilipofikia wengine wenu
Hawatafika.

Kula nimekula na sasa mwasema
Niko nyuma ya wakati
Lakini kama mngepita mbele
Na uso wangu kuutazama
Ningewambia siri ya miaka mingi.

(a) Haya ni mashairi aina gani? (alama 1)

(b) Washairi hawa wawili wanalalamika. **Yafafanue** malalamishi yao. (alama 4)

(c) **Onyesha** vile kinaya inavyojitokeze katika tungo hizi mbili (alama 4)

(d) Ni vipi Hadija:
(i) amekata mti mtima?
(ii) amepita nyuma ya Punda? (alama 4)

(e) Kwa kurejelea shairi ‘B’ **eleza** maana ya:
(i) mzigo
(ii) siri
(iii) Niko nyuma ya wakati (alama 3)

(f) **Andika** ubeti wa kwanza wa shairi ‘ A’ kwa lugha nathari. (alama 2)

(g) Uhuru wa mshairi umetumiwa vipi katika shairi ‘B’ (alama 2)